
UTANGULIZI

Kitabu hiki nilikiandika mnamo mwaka 2003 nilipokuwa ninafundisha shule ya sekondari Busolwa iliyoko Wilayani Nyang'hwale mkoani Geita. Kwa sababu mbalimbali sikuweza kukichapisha mpaka sasa miaka kumi baadaye.

Natambua baadhi ya matukio yaliyosimuliwa ndani ya kitabu hiki yamekwisha kupitwa na wakati hasa mandhari ambayo kwa hakika yamebadilika mno. Lakini hata hivyo hii ni hadithi ya kubuni, na hivyo ninayo imani kwamba maudhui yake hayajapoteza maana kwa wasomaji wangu wote wa wakati huo na wale wa sasa.

Ni matumaini yangu makubwa kuwa, kuchelewa kuchapwa kwa kitabu hiki ulikuwa mpango wa Mungu ili kuwakumbusha watu wengi walioufahamu mji wa Geita miaka kumi iliyopita na kuwapatia fursa ya kutathmini maendeleo tuliyoyafanya wana-Geita kwa muda mfupi huu katika maisha.

Haiyumkiniki pia kitawafundisha mambo kadhaa wasomaji wangu ambao miaka hiyo ama walikuwa watoto wadogo sana kiasi cha kutokutambua jambo au hawakuwako kabisa ulimwenguni humu.

Niwatake radhi wote kama kwa namna moja ama nyingine nitakuwa nimewakwaza katika kuwakumbusha yaliyopita.

Nikidaiwa kutoa shukurani kwa watu wote walioingiza jitihada yao kwenye ukamilishwaji wa kitabu hiki, siwezi kuwataja wote hapa kwa sababu ya kukwepa kukikuza mno na hatimaye kikatugharimu pesa nyingi kukikamilisha.

Ninawiwa hata hivyo kuwataja wachache ambao mchango wao umekuwa mkubwa mno mpaka ninahemewa.

Wa kwanza ni marehemu Baba yangu Mwalimu *Amos Haji Yona* ambaye mpaka umauti unamfika alikuwa katika jitihada ya kuhakikisha wanawe tunapata elimu. Pumzika kwa amani Baba Yetu nasi deni hilo tunazidi kumwomba Mungu atupe nguvu ya kulitimiza – tutawasomesha wanetu.

Wa pili ni Mwalimu *Danlop Otieno Ochieng* wa chuo kikuu Dar es Salaam ambaye hakika miaka ile tukiwa naye Busolwa, ndiye aliyegundua kipaji changu katika uandishi—akanihimiza kuandika.

Tatu ni yule yule ambaye huwa siachi kumtaja—msaidizi wangu katika kazi zote—mwenzi wangu wa maisha—mke wangu kipenzi *Regina*.

Siwezi kuwasahau wafanyakazi wenzangu pale VETA–Kagera, hakika hamasa yao kwangu imekuwa kubwa mno. Nawashukuru kwa ujumla wao.

Mwisho, Mungu Baba wa mbinguni, uliyumba viumbe vyote, ukapenda nami niwepo na ukanipa hata kipaji hiki cha kuandika. Asante Mungu wangu, bariki kazi ya mikono yangu, bariki hata uzao wangu, uwape neema ya kukutumikia.
Aamin!

Samwel B. Mayala.
Julai 2014
Bukoba—Tanzania.

